# *Ono Ni Nini?*

Asanteni, sana. Twaweza kuomba?

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa wema Wako wote kwetu. Mungu, tunajiona tu hatufai, na kutazama kusanyiko hili leo na kuona keki hii ya siku ya kuzaliwa imewekwa hapa. Samahani, Baba. Unisamehe. Kamwe siwezi kuzungumza. Lakini naomba, Mungu, ya kwamba kwa namna fulani, kwa namna fulani, kwamba mkondo huu wa upendo wa Kiungu utamsaidia tu kila mtu. Wabariki watu hawa waliolifanya jambo hili kuu, Baba. Ninaomba tu kwamba baraka Zako zitakuwa pamoja nasi, kuu sana, leo, mpaka jengo lote litafurika kwa Utukufu Wako. Na—na uwazie wakati ule ule kuwatazama wale viziwi na mabubu wanaopita, wakienda ng'ambo ya pili. Loo, naomba, Mungu, kwa namna fulani, tenda jambo fulani kwa njia kuu leo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

3 Baraka za Mungu na ziwe juu ya Buckman. Naomba tu kwamba Mungu atawabariki, rafiki zangu wapendwa. Hilo ndilo jambo zuri zaidi. Nadhani . . . Je, umeionyesha kwa umma? Wameiona? [Ndugu fulani anasema, "Naam."—Mh.] Naam. Si ni zuri hilo? Nataka kuchukua wakati huu kuwashukuru. Hakuna njia ulimwenguni ambayo ningeweza kumlipa yeyote wenu baraka zenu za fadhili. Nami niliona zawadi nilizokabidhiwa, halafu zile zawadi ndogo katika bahasha, na kadi na kadhalika. Ajabu sana! Inanifanya tu kujisikia kama nataka kuweka miadi, kurudi mwaka ujao kwa ajili ya siku ya kuzaliwa kwangu. [Kusanyiko linashangilia.] Asanteni, sana. Jamani! Hilo ni zuri sana. Nilitazama pande zote; sikujua hiyo ilikuwa ni nini. Na hakika inapendeza, na zawadi zenu zote.

4 Kuna kitu kimoja tu ninachoweza kusema. Na hiki si hasa . . . Vema, ni kusema kwa maombi, "Mungu awabariki." Na kama nisipoweza kamwe . . . wala Mungu asiniruhusu nilifanye katika maisha haya, ku—kuonyesha shukrani zangu kwa zawadi hizi zote kutoka kwa kila mtu. Hata msichana mdogo alikuwa na bahasha ndogo mle ndani, nayo ilikuwa ni zaka zake, za takriban senti nane, nadhani ndivyo ilivyokuwa. Alinitumia kama zawadi ya siku ya kuzaliwa, zaka zake. Kuanzia hiyo, hadi kwenye zawadi hizi kuu hapa, loo, Mungu awalipe vikubwa, ndugu na dada zangu wapendwa. Ninaninii tu . . . Sikufikiri kweli mliniwazia kiasi hicho. Kweli sikuwazia. Ninalithamini.

5 Leo, ni—ni, tumelichukua kwa mazungumzo ya moyo kwa moyo, naamini, leo. Ni, badala ya kuhubiri ilikuwa ni kuzungumza tu na labda tueleze baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuonekana kuwa ya ajabu sana kwenu mikutanoni.

Kidogo nimeishiwa na pumzi. Ninii tu, sikutarajia siku nyingine ya kuzaliwa leo.

6 Ndipo nikiingia tu mlangoni, nilikutana na rafiki yangu mwema hapa, Art Wilson. Nadhani wafanyabiashara Wakristo wote wanamjua. Nyumba ya—yako iko Oregon, sivyo? Au . . . [Ndugu Wilson anasema, "Reno, Nevada."—Mh.] Reno, Nevada. Ndugu Art Wilson, kwenye mkono wangu wa kulia.

7 Mtu anayefuata ni Bw. Wood. Bw. Banks Wood, ni rafiki na jirani yangu. Bw. Wood amekuwa akiambatana nami. Na wengi wenu ninyi watu mnamjua, kwa kuuza vitabu mkutanoni. Mtu huyu amekuwa mkandarasi aliyefanikiwa sana. Basi siku moja, nilipokuwa Louisville, Kentucky, nikiwa na mkutano; yeye mwenyewe akiwa Shahidi wa Yehova, mke wake akiwa Mmethodisti. Walikuwa wamesikia habari za huo mkutano, kwa hiyo wakaendesha tu gari na kuja ili kuona jinsi ulivyokuwa wa kweli.

8 Usiku huo, kulikuwa na msichana aliyekuwa amelazwa kwa miezi kadhaa, hawezi hata kusogeza kiungo chochote, kuanzia nyonga yake kwenda chini. Msichana wa takriban, loo, binti wa takriban umri wa miaka kumi na mitano, akainuka moja kwa moja kutoka kwenye machela yake, jinsi alivyoletwa jukwaani, akatembea kote mahali hapo. Kesho yake, akaendelea tu. Akarudi shuleni baada ya siku chache; ni mzima kabisa, bado. Na mambo mengi Bwana aliyafanya.

9 Kwa hiyo Bw. Wood, akiwa na jambo la kufanya . . . nyumba ya kumalizia, ama kitu fulani alichokuwa akifanya, ilimbidi kuharakisha na kulikamilisha; akaenda Houston, Texas, kwenye mkutano wangu uliofuata. Huko, alikuwa amesimama chumbani usiku huo wakati Malaika wa Bwana alipotokea, nazo kamera zikapiga picha ya huyo Malaika, ambayo, ile picha ambayo umeiona, wewe mwenyewe, hapa.

10 Halafu, alikuwa na mmoja wa mibadala yake mikuu. Alikuwa na mvulana aliyelemaa, nao mguu wake umekunjamana chini yake. Ndipo Bw. Wood, niliporudi . . . Nilienda ng'ambo, na huko Uswidi; nikarudi. Ndipo wakaweka hema ndani, naamini ndivyo ilivyokuwa, Cleveland au . . . Cleveland, Ohio. Naye Bw. Wood, hata hivyo, bila shaka akiwa kwenye huo umati, akifuatilia tu, kama wengi wenu mlivyo bado leo, lakini akidhamiria kukaa hadi imalizike. Hiyo ndiyo njia, njia ya kufanya. Basi akaweka kando kazi yake na kumleta huyo mvulana hadi Cleveland.

11 Baada ya siku chache usiku, hiyo ilikuwa mkutanoni. Bila shaka, sikumbuki; ila tu kwa kanda. Alikuwa ameketi nyuma katika hema, nyuma kabisa, yeye na mkewe. Ndipo Roho Mtakatifu akashuka na kusema, "Mwanamke huyo aliyeketi hapo nyuma na mumewe, mkandarasi," kasema, "yeye mwenyewe ana uvimbe. Na mvulana wake amelemaa. Lakini,

BWANA ASEMA HIVI, 'Ameponywa.'" Wakamwinua maskini huyo jamaa mdogo. Yuna mguu mchanga, mzima, ulionyooka, tangu saa iyo hiyo na kuendelea, kawaida tu vile mvulana yeyote angeweza kuwa.

12 Bw. Wood akaacha ukandarasi, anazurura-zurura pamoja nami. Kwa hiyo, mvulana wake na mvulana wangu ni marafiki wasiri sana, pamoja. Naye ni mzima tu na mwenye afya kama mvulana yeyote, akitarajia kwenda jeshini moja kwa moja. Kwa hiyo Bwana ni mwema, sivyo? Na mwingi wa rehema. Na ni mambo mangapi makuu ambayo amefanya miongoni mwetu!

13 Sasa, leo, sasa, usiku wa leo, nafikiri, kwa kuwa . . . Tutaanza mapema kidogo. Sina budi kuwa Louisville, Kentucky, kwa miadi asubuhi, saa mbili, na sina budi, kuendesha gari umbali huo wote, usiku wa leo, ambao ni kuendesha gari saa nane ama kumi. Kwa hiyo, tutafika huko kwa wakati mzuri wa kutimiza hiyo miadi. Tutaondoka moja kwa moja kutoka hapa, hadi . . . kwenda Louisville, na kwa gari. Halafu tunakusudia kuanza ibada mapema kidogo, usiku wa leo. Nasi tunathamini kujitokeza kwenu, mapema kidogo, tafadhalini. Waliniambia naweza kuwa jukwaani . . .

14 [Ndugu Joseph Mattsson-Boze anasema, "Kadi zitasambazwa saa kumi na mbili."—Mh.] Kadi zitatolewa saa kumi na mbili, Ndugu Joseph alisema. Nasi tulikuwa tu . . .

15 Jeshi linaweza kumchukua Billy hivi karibuni sana, kwa hiyo Bw. Wood anasambaza kadi za maombi, naye Billy anamsaidia. Nikasema, "Unaendeleaje, Bw. Wood?"

16 Akasema, "Aisee!" Akasema, "Ni sawa, lakini," kasema, "nilisaliwa na kadi mbili na kulikuwako na watu sita waliozitaka." Hiyo ni . . . Akasema, "Unafanya nini katika hali hiyo?"

Nikasema, "Yale tu uliyofanya." Nikasema, "Vema, yeye . . . "

17 Ndipo jana usiku, alipokuwa na furaha sana, alisema, kuwaona hao watu a—aliokuwa amewapa hizo kadi, wamesimama jukwaani, huku Mungu akiwaponya na kuwapa afya. Basi alifurahi sana juu ya hilo!

18 Sasa, usiku wa leo, zitasambazwa saa kumi na mbili, kwa sababu nafikiri ninapaswa kuwa jukwaani saa mbili kasorobo. Ninaamini hiyo ni kweli. Halafu basi, ili tuweze kufumukana mapema kidogo, kwa sababu ya usafiri mrefu kwa gari, wenye kuchosha usiku wa leo.

19 Kwa hiyo, asanteni, kwa kujitokeza, alasiri ya leo. Na kwenye alasiri hii yenye upepo, baridi, na hata hivyo mkaja. Inaonyesha hamji mpate kuonekana. Mnakuja kwa ajili ya mema mnayoweza kupata mkutanoni, kutoka kwa Mungu. Nami naomba kwamba Yeye atawabariki, kwa wingi.

Sasa, hasa, haimaanishi watu wanapaswa kuwa hapa saa kumi na mbili; ni ninyi tu mnaotaka kadi za maombi.

20 Na sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusanyiko letu kwa jumla. Nami na—natumaini ya kwamba siku moja, Bwana akipenda, kurudi Chicago hivi karibuni tena, na kumtumikia Bwana.

Biblia ilisema hapa:

> *Akiwapo miongoni mwenu* mtu wa rohoni au *nabii,*
> *Mimi Bwana nitajitambulisha kwake* katika maono, . . .

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake. Sasa, kama tu mazungumzo ya moyo-kwa-moyo. Nitaninii . . .

21 Joseph hajui hili. Lakini nitamwomba tu kama, wakati wowote, atanikatiza wakati nikizungumza, na aseme lolote. Tulikuwa na mahojiano ya kitu kama hiki, asubuhi ya leo, kwenye redio. Nyote husikiliza kipindi hicho? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

22 Na—na hivyo basi, kufikia—kufikia leo hii, nilifikiria, labda kwa namna fulani kupata tu hi—hisia za watu, ili mweze kuona huo, huo utendakazi wa mambo ya kimbinguni. Nami nifanye tu mazungumzo ya moyo-kwa-moyo sisi kwa sisi, niwaruhusu mwingie ndani ya Hili, kadiri tu niwezavyo kwenda. Wala sijawahi . . . Mengi ya mambo haya niliyo nayo moyoni mwangu kuyasema, sijawahi kuwaambia wasikilizaji hapo kabla, maishani mwangu. Basi na aongeze baraka Zake kwa yale tusemayo.

23 Jambo la kwanza tunalotaka kuzungumzia ni: *Ono ni Nini?* Lingekuwa ni nini? Baadhi, watu wengi sana . . .

Sisemi, kama Ndugu yetu Billy Graham alivyosema, "Kuwajibu wakosoaji wangu." Ninashukuru sana nina wakosoaji wachache sana. Karibu kila mmoja . . .

24 Baadhi yao ambao hawajawahi kufika mkutanoni wanaweza kusema, "Loo, vema, hakuna kitu hapo." Lakini mara wakiwa mkutanoni, sikuzote karibu linatatuliwa, wakati Yesu anaposhika moyo wao, nao wanaona basi kwamba ni—kwamba ni kweli.

25 Ono ni—ni ninii tu . . . Watu wengi huniuliza, "Ndugu Branham, je, ni kitu halisi unachotazama? Au, ni hisia tu juu ya akili? Au, ni nini?" La. Ni halisi. Ni kama tu vile ninavyoangalia sasa hivi.

26 Na sasa, jinsi hilo linavyotukia, linafanywa kwa neema kuu ya Mungu. Na wakati nilipokuwa mtoto tu, hapo nilipozaliwa, mama yangu huniambia kwamba Nuru hii iliingia na kuning'inia juu ya kitanda kidogo nilimozaliwa. Na halafu, tangu ninavyoweza kukumbuka, mambo hayo yametukia mbele yangu.

27 Linaninii tu, linafunguka tu. Inaonekana tu kwamba hakuna njia ningeweza kulielezea; bali, ili kupata tu yaliyo bora zaidi niwezayo: najitolea tu kwa Roho Mtakatifu. Nalo linaanza tu, na hilo hapo mbele zako. Unajua kuwa umesimama hapa, na hata hivyo uko miaka arobaini huko nyuma katika maisha ya mtu fulani, ukiangalia wanachofanya. Na halafu, jambo pekee ninalosema, ni kile tu ninachoangalia.

28 Ndipo kidogo ninapojirudia mwenyewe, ninagundua kwamba nimesema jambo fulani, lakini mara nyingi sijui nilichosema. Na jinsi ninavyolipata, ni hawa wavulana, hao wanaoketi hapa chini, vinasa sauti hivi, wananichezea tena. Basi hivyo ndivyo ninavyolichukua. Kwa hiyo, haliko ndani yangu mwenyewe, hata kidogo.

29 Halafu hilo—hilo linatolewa kwa kusudi mo—moja. Sasa, nafikiri, nami nasema hivi kutoka moyoni mwangu, kwamba utaratibu ulio mkuu na wa juu sana uliopo wa Mungu kuwapa watu Ujumbe Wake, ni kwamba watu waliamini Neno Lake. Hiyo ni kweli. Huo ndio utaratibu wa juu zaidi. Kuhubiri Injili ndio utaratibu wa juu zaidi. Ndipo, mkiangalia, Biblia inaliweka hivyo. "Wa kwanza ni mitume, wa pili nabii," na kadhalika, kisha kushuka chini, chini, hata unaingia katika zile karama tisa za kiroho zinazotenda kazi katika kila mwili wa mahali hapo.

30 Sasa, huduma zangu Marekani hazijakuwa nzuri sana kama zilivyopaswa kuwa, huku Marekani. Huduma zangu zina nguvu zaidi, kwa ajili ya Bwana, huko ng'ambo. Wanaziunga mkono vizuri zaidi. Sasa, sijui ni kwa nini. Sasa, sizungumzi juu yenu watu. La. Ninazungumza juu ya umma kwa jumla, mnaona, kila mahali, kama vile Chicago, kwa jumla, tungesema; au—au, Durban, Afrika Kusini, kwa jumla, mnaona, kitu kama hicho; au, Jiji la Meksiko, kwa jumla. Vema, wataziitikia, asilimia themanini zaidi ya watakavyoziitikia huku Marekani.

31 Sasa, kile kinachowavutia Wamarekani zaidi, ibada za uponyaji, kwa maoni yangu, ni, vema, za Ndugu Oral Roberts. Sasa, Ndugu Oral Roberts ni mnenaji hodari, mhubiri halisi, na ndugu mwema mcha Mungu, ndugu yetu, Oral Roberts; na rafiki msiri wangu, ndugu mpendwa. Nami nina heshima kuu, za kilindi kwa Ndugu Roberts. Naye Bwana yu pamoja naye na anambariki, mno, na mikutano yake hapa Marekani. Yeye. . .

32 Sote wawili tunaweza kwenda kwenye mji, naye angeutayarisha mkutano wake, nami niutayarishe mkutano wangu. Kusanyiko lake lingelizidi langu kwa mbali, mara nyingi, kwa tangazo dogo tu, kwa sababu huduma yake ina matokeo makubwa zaidi hapa Marekani, kwa sababu yeye ni m—m—mnenaji mwenye ushawishi sana. Yeye ni . . . Naye ana nji—njia. Yeye ni mwerevu na mwenye elimu, na anaijua Biblia. Naye anaweza kuiwasilisha kwa namna ambayo watu wenye

elimu wanaisikiliza hiyo, kwa sababu hiyo iko kwenye kiwango ambacho wana—wanaishi.

33 Lakini hebu tuchukueni sisi, wakati tulipoenda Afrika, vema, hapakuwa na mfano wake, hata kidogo. Mnaona? Nao watu wasio na elimu, na kadhalika, huyatafuta mambo ya kimbinguni, kwa sababu hawana hii, elimu na . . . hawajafunzwa kielimu kama watu hawa hapa. Hivyo basi ninii . . . Ni kitu ambacho Bwana ametoa, kuwavutia watu.

34 Sasa, simaanishi kusema kwamba . . . Watu wengi wasomi, werevu, wenye akili, baadhi ya walio juu sana, hata kufikia wafalme, watawala, wakuu, bila shaka, wanaliamini na kulipokea.

35 Lakini kwa jumla, makanisa yetu ya Marekani, imekuwa muda mrefu tangu tulipokuwa na uamsho, kutoka huko nyuma kabisa katika wakati wa Wesley. Vile vizazi vya kale vilififia. Wakati, watu wa Wesley walikuwa wakifukuzwa na kuitwa "watakatifu wanaojibingirisha" na "wagutukaji," kwa sababu walitikisa vichwa vyao, na—na kulala kwenye ninii . . . kwenye majukwaa na kila mahali, kwenye marefu ya kanisa. Waliwamwagilia maji na kupepewa, wakati Roho Mtakatifu alipowashukia. Sasa, siku hiyo imekwisha, muda mrefu uliopita.

36 Sote tumetulia kwenye, loo, Orthodoksi sana. Lakini hiyo ndiyo sababu hawawezi. Watu siku hizi wanafundishwa, vema, m—mzungumzaji anayeweza kuliwasilisha kwa—kwa ustadi sana. Vema, hilo ni sawa tu. Hilo ni sawa tu kabisa. Na mradi tu unampokea Kristo, hilo ndilo—hilo ndilo jambo kuu, mradi tu unampokea Kristo.

37 Sasa, tunamwona Ndugu yetu Roberts. Mlisikia kipindi chake asubuhi ya leo, labda. Nami nilisoma yale makala gazetini, na nikaipata mwenyewe. Kuanzia jinsi ambavyo . . . Na huko Australia, ni jambo la kuchukiza jinsi gani, wao wakimzomea, wakimwita "bandia" na kila kitu, na kumfukuza namna hiyo. Ambako, labda ninii . . . aina hii ya huduma ingenyamazisha jambo hilo, sasa hivi. Mnaona? Mnaona? Ingekuwa tofauti. Na, lakini, Ndugu Roberts, hata hivyo, Mungu amempa njia ya kufanya kazi na watu ambao nisingeweza kuwagusa. Na labda mimi ninafanya kazi na watu ambao yeye hawezi kuwagusa. Lakini, pamoja, sisi ni ndugu tunaojaribu kufanya tuwezalo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Mnaona?

38 Na maono ni sehemu tu ya Injili inayohubiriwa. Sasa, mnaona, kama ningalikuwa na elimu na pengine ningekuwa na sauti nzuri, na kadhalika, na ningaliweza kuwasilisha Injili, kama, pengine ningekuwa m—mhubiri wa aina hiyo. Lakini, Mungu akijua ya kwamba sitaelimika, ilimbidi anipe kitu kingine cha kufanyia kazi, mnaona. Na hivyo ndivyo alivyofanya, jambo pekee nilijualo.

39 Sasa, huenda mkashangaa ni nini kinachotendeka jukwaani. Wakati m—m—mgonjwa au. . .Nisingelisema hivyo. Hilo limezidi sana katika msamiati wa matibabu. Naomba niseme, wakati rafiki anaposimama mbele yangu, akitaka usaidizi, haya ndiyo yanayotendeka. Sina uhusiano wowote na hilo, hata jambo moja. Mgonjwa huyo mwenyewe ndiye anayeitumikisha karama hiyo ya Kiungu. Sina uhusiano wowote nayo, hata kidogo. Ninaendelea tu kujitolea, kujitolea, mpaka roho yao na Roho aliye juu yangu, ambaye nimejitolea kwake, mpaka Roho Mtakatifu. . .

40 Nitaliita hivi, nilifanye hivi, hasa, ili mpate kuelewa. Huyu hapa Roho Mtakatifu *hapa* juu, halafu ninaendelea tu kujitolea Kwake, mpaka nijue ya kwamba Yeye—Yeye yupo. Nami ninazungumza na huyo mtu mpaka nipate usikivu wao. Hadi wakati huo, sijui lingine. Ndipo Roho Mtakatifu, kwa kujitolea roho yangu, ananionyesha maisha yao. Basi hilo linapotukia, hilo hujenga imani ya huyo mgonjwa, hadi mahali kama hapa.

41 Na mara nyingi, basi, ninaanza kusema jambo lingine, Naye atanizuia na kusema, "BWANA ASEMA HIVI." Sasa angalieni hilo. Hilo ni kamili, kila wakati. Halijapata kushindwa. Litawaambia tu kile kinachokaribia kutokea. Na itakuwa hivyo. Liandikeni chini, na muone kama sivyo lilivyo.

Sasa, huyo, huyo mgonjwa anafanya hivyo.

42 Sasa naweza kutoa hili katika mfano mdogo tu wa kielimu, ili mpate kuelewa. Tuseme, huko, kuna ninii kubwa sana. . . Sisi sote ni wavulana na wasichana wadogo, nasi tuko huko chini kwenye. . .huko nyuma katika wakati wa ujanani. Na kuna ua mkubwa tu hapa. Kuna kanivali mle ndani. Nami ni—ni—nitokee tu kwamba ni mrefu kidogo kuliko wewe. Labda una nguvu kunishinda, lakini mimi ni mrefu zaidi. Unaona? Mungu huumba watu kwa njia tofauti kwa kazi tofauti. Vema, basi, huko *juu* kabisa, karibu na mahali ninapoweza kuchungulia, kuna shimo ukutani. Vema, sasa, ninaweza kushika juu, kwa sababu ni mrefu kidogo, na ninaweza kujinyanyua, kwa vidole vyangu, na kuchungulia kwa tundu hili. Nirudi na kukwambia nilichoona. Mnapata hilo wazo sasa? Mnanifuata?

Sasa, sasa, labda mtu anayefuata, ana nguvu zaidi, lakini hawezi kuona parefu hivyo. Kwa hivyo atasema, "Ndugu Branham, unaona nini?"

43 Nitasema, "Ngoja kidogo." Nami nitaruka juu, juu sana, na kushika juu kwa vidole vyangu, na kujivuta, mzito sana. Nami nitasema, "Na—na—naona ndovu." Kisha nashuka. Mnaona? Inachosha, kwa sababu ninajinyanyua. Ninasema hivi katika mfano mpate kuelewa.

Sasa, ninaposhuka chini, "Umeona nini?"

"Ndovu." Mnaona? Vema.

44 Sasa, hiyo ni kama mtu anayesimama jukwaani, akitumia kipawa cha Kiungu, linachosha, kwa sababu huyo mtu ndiye anayetumikisha karama hiyo. Hawaijui hiyo, bali ndio wanaoitumikisha, wao wenyewe.

45 Sasa, niliambiwa jana usiku ya kwamba kulikuwa na mtu aliyesimama jukwaani. Ndugu Joseph aliniambia, baada ya kukutana nami, kwamba mtu huyo alikuwa . . . Mimi . . . Kwanza, alipokuja huku, nami nilifikiri alikuwa kiziwi na bubu. Nikasema, "Unaendeleaje, bwana?" Kitu kama hicho. Huenda nisilinukuu vema. Ninachukua yale waliyoniambia. Sijawahi kuisikiliza hiyo kanda bado. Naye akasema mtu huyo alisimama tu pale. Nikasema, "Vema, labda yeye ni kiziwi na bubu."

46 Na sasa angalieni neema kuu. Mnaona? Hiyo ni kama yule mwendawazimu jukwaani. Hiyo ni kama vile mchawi Afrika, akisimama pale na mifupa vidoleni mwake, kukupa changamoto, unaona. Neema inashikilia basi. Huna haja ya kuhofu. Usihofu. Hamna hofu kwake. Neema inashikilia. Mungu hushikilia pale ambapo huwezi kushikilia. Na ndipo basi mtu huyo alipokuwa amesimama pale. Kabla . . . Ni—nilisema, "Vema, labda yeye ni kiziwi na bubu." Na kwa ghafla, likatokea ono mbele yangu. Kisha . . .

47 [Kengele ya saa ya Ndugu Branham inalia—Mh.] Sasa, samahani saa hiyo inalia. Hiyo ilikuwa ya kufika . . . kuja huku na kuanza. Kwa hiyo, nilijua umeichukua kwenye hili. Ndio kwanza wanipe saa ya mkono kule, inayopiga kengele. Kwa hivyo, huo sio wakati wa kusimama bado, natumaini. Basi katika . . . Nitaisikia hii; usijali.

48 Kwa hiyo, basi, mtu aliyesimama pale. Lile ono, upesi, pengine, niliona Ufini ama chochote kile. Sikumbuki. Lakini sasa, chochote kile, walisema nilimwambia kwamba yeye alikuwa Mfini. Naye anatupumbaza, kitu kama hicho, labda alikuwa Mfini. Vema, Joseph hapa, alisema angeweza . . . Hilo lilikuwa jambo la ajabu sana kwake, jinsi lingejua mtu huyo alikuwa wa taifa gani. Mungu katika neema Yake alionyesha hilo.

[Ndugu Joseph Mattsson-Boze anazungumza na Ndugu Branham kuhusu yule ndugu wa Kifini aliyeponywa—Mh.]

49 Sijui kama kuna uwezekano mtu huyo angekuwa humu jengoni leo, na kama mtu fulani ameketi karibu naye, ambaye kwa namna fulani . . . kama wangeweza kuzungumza Kifini, wange—wangeona . . . Kama hiyo ni kweli, waweza kuinua mkono wako? ikiwa huyo mtu yuko jengoni, leo, yule Mfini aliyekuwa hapa jana usiku, ambaye tunazungumza habari zake, aliyekuwa jukwaani. Nilitaka tu—nilitaka . . .

50 [Ndugu Joseph Mattsson-Boze anaendelea kuzungumza na Ndugu Branham kuhusu yule ndugu wa Kifini aliyeponywa—Mh.] Vema, hilo, nadhani alirudi, labda, nyumbani kwake.

51 Sasa, sasa, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, na ninii . . . Alikuwa Msemaji wa Mungu aliyepakwa mafuta. Je, mnaamini hilo? Alikuwa Mwa—Mwana wa pekee wa Mungu. Naye Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, pasipo na kipimo. Unaamini hilo, mwanafunzi wa Biblia? Alikuwa ni Emmanueli. Hakuna hata mmoja wetu atakayewahi kufika mahali hapo. La. La. Alikuwa Mwana mtakatifu wa Mungu aliyezaliwa na bikira, nasi hatutakuwa kamwe. Kamwe hatutaweza kufanya hayo mambo, namna hiyo, kwa maana Yeye alikuwa Huyo.

52 Lakini sasa aliahidi ya kwamba mambo aliyofanya sisi nasi tungeyafanya, kwa sababu tungefanywa wana wa Mungu wenye mamlaka, kupitia Kwake. Hiyo ni kweli? Sasa, hilo si ninii . . . Hilo ni kwa ajili ya kila mmoja wetu. Kila mwaminio anakuwa wana na binti za Mungu. Hiyo ni kweli?

53 Sasa, wakati yule mwanamke mwenye kutokwa na damu alipoligusa vazi Lake, hiyo ilikuwa tu ni kama kule kuchungulia tunduni. Unaona? Alihisi nguvu zilimtoka. Akawa—akawa dhaifu, lakini hakujua kilichotokea. Mtu fulani alikuwa amemgusa, kwa i—imani. Naye akauliza ni nani, na kila mtu akakana. Kwa hiyo basi kilichotukia baada ya Yeye kufanya hivyo, mbona, Yeye aliangalia pande zote mpaka akaona. Sasa, kuna ninii . . .

54 Je, alimjuaje? Hilo ndilo swali ninalotaka kuwaletea. Je, alimjuaje? Sasa hebu nijaribu, kwa . . . kama ndugu, kueleza hili, jinsi Yeye alivyomjua.

55 Kwa sababu, wakati mtu yeyote amefanya hivyo, naweza kusema kutoka mikutanoni hapa, kutokana na utendaji wa Roho Mtakatifu. Wakati mtu yeyote amebarikiwa, inaonekana tu kama ni kitu fulani kinachokuvuta, namna *hiyo*, unaona, nawe unamfikia mtu huyo. Halafu basi, juu tu ya mtu huyo, unawaona na kile kilichowapata, na kwamba wana shida gani. Halafu unaangalia, nawe unaona ni mtu yule yule, na ni kama tu nji—njia au mfereji ambao unafanya kazi kati yako na mtu huyo.

56 Hivyo ndivyo ninavyowazia. Kamwe Yeye hakulielezea. Hivyo ndivyo ninavyowazia kwamba Yeye alijua jambo hilo. Kwa sababu, Roho Mtakatifu akitenda kazi kwa njia kama hiyo, hivyo ndivyo linavyoeleweka.

57 Tuseme, kama wakati mwingine unaposema, "Yule mwanamke anayeketi pale, ambaye amevaa kofia ya kijani," au kitu kama hicho, "umekuwa ukiugua *ninii*. Unatoka mahali *fulani*." Unasikiliza hilo. Unaona? Uko moja kwa moja katika ono, ukiangalia kile kinachotendeka. Na halafu labda unamwona akirudi nyuma, na amezungukwa na nuru, na kila kitu. Mbona, ndipo unasema, "Mbona, ameponywa. Ni BWANA ASEMA HIVI." Unaona? Bwana ambaye anaonyesha hilo ono, ni imani yako tu Kwake, ananitumia kama msemaji kukwambia

yale unayotamani akwambie. Unaona ninachomaanisha? Sasa, lakini wakati ni ile nyingine . . . Sasa, hiyo ni njia tu ya kuruhusia ya Mungu, ikifanya kazi.

58 Nasema hivi kwa heshima. Saa imekaribia, wakati mimi . . . nikiisha kuwaambia lile ono ambalo Bwana amenionyesha, kwamba hii hatimaye itarudi nyuma, ikitoa nafasi kwa kitu kilicho bora zaidi. Na hilo ndilo ninalotaka kufikia, alasiri ya leo.

59 Sasa, mtu anayefanya hivyo, ata—ataninii, endapo wataliamini, watabarikiwa na watapata afya. Sasa, si kwamba waliponywa; lakini imani yao ilimgusa Mungu nao wakakubali uponyaji wao ambao tayari ulitolewa kwa ajili yao, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Unaona? Si kwamba hiyo ilikuwa na uhusiano wowote na uponyaji wao. Ilikuwa tu ni msemaji, kunena.

60 Ilikuwaje popote katika Biblia? Hatuninii . . . Sijilinganishi na nabii. La, bwana. La. Mimi ni maskini mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Lakini karama ambayo Bwana aliwapa manabii, na kuwafanya manabii, walikuwa wasemaji wa Mungu. Walikuwa na Neno la Bwana. Wala hakuna nabii aliyewahi kufanya lolote kwa matakwa yake mwenyewe. Alifanya hivyo, kwanza, baada ya Mungu kumwambia. Hiyo ni kweli.

61 Na hivyo ndivyo Mwana wa Mungu, alipokuja, ambaye alikuwa ni Mungu wa nabii. Alisema, "Ninafanya tu kama vile Baba anavyonionyesha kufanya." Hiyo ni kweli. Inabidi tu ije kupitia kwa nguvu za Kiungu, kufunua kupitia mwili. Naye Kristo alikuwa Msemaji wa Mungu duniani. Kila mtu anaelewa hilo?

62 Sasa, kwa mfano, wakati mwingine, nitakuwa nyumbani. Gene, Leo na hao wengine niliokuwa nikiwazungumzia jana usiku, wanaoketi hapa chini, Ndugu Beeler na wengi wa hao wengine, na wale wanaonijua. Nyumbani, nitakuwa nikitembea kote nyumbani, bila kufikiria chochote. Labda niketi chini chumbani, ndipo litatokea ono. Na labda litakaa kimya kabisa kwa muda kidogo. Kisha litasema . . .

63 Atasema, "Sasa, utapigiwa simu katika dakika chache, kutoka kwenye simu, nawe utaingia katika mji *huu*. Basi ukiingia kwenye mji huu, utaenda mahali *fulani*. Itakuwa *hivi*. Nawe utaingia chumbani, kisha utaweka kofia yako chini. Au, huyo mama ataweka kofia yako juu ya kitanda, lakini haipaswi kukaa hapo. Inapaswa kuwekwa mezani, ndipo mwanamke mwingine ataingia *hivi*."

64 Utaona yote yakitekelezwa hasa jinsi yapaswavyo. Basi kama nikishindwa katika moja ya mambo hayo, halitatukia. Haina budi kuwa katika muda na wakati kamili, na kila kitu kiko mahali pake kabisa, kwa maana ni ono. Ha—

halina budi kutokea kikamilifu. Ndipo basi linapotokea, halina budi kutukia. Halijawahi kushindwa. Sasa, hapo ni wakati Mungu anapotumia karama Yake. Hilo halinidhoofishi. Hilo halinisumbui.

65 Sasa, Yesu alipomfufua Lazaro kutoka kaburini, ulikuwa ni mwujiza mkubwa kuliko yule mwanamke aliyeligusa vazi Lake na akaponywa kutokwa na damu. Je, mnakubali hilo? Kamwe hakusema neno moja kuhusu kudhoofika, na nguvu kumtoka, kwa sababu Mungu alikuwa akitumia karama Yake. Mnaona? Hayo ni aina hiyo ya ono. Hilo ni ona la namna hiyo.

66 Lakini watu wanapoitumia karama ya Mungu, na kinachonidhoofisha hivyo, jukwaani, ni wewe mwenyewe. Hicho ndicho kinacholifanya. Wewe mwenyewe ndiye unayeifanya hiyo kazi, kuitekeleza, ndiyo sababu inavuta. Ama ni wewe ukiitumia karama ya Mungu, au Mungu akitumia karama Yake.

Sasa, kwa kulinganisha, ningesema . . . Kama ungeniuliza, "Kuna nini huko?"

"Naam, ni twiga."

"Umeona nini kingine? Nini . . . ?" Unachoka, unaona, ni kitu kingine unachoona.

67 Lakini sasa Mungu anapotaka ujue kinachotokea, Yeye anakunyanyua tu na kukuinua juu ya kitu hicho chote, na kusema, "Hii hapa sarakasi yote. Unaona? Hii ndiyo picha nzima. Utafanya *hivi*, na kufanya *hivi*, na kufanya *hivi*, na *vile*." Anakuketisha chini. Amekuinua, kwa mikono na bawa Lake la milele. Wala hakuna kitu duniani . . . Unarudi chini, unajisikia kupiga kelele za ushindi. Lakini ndivyo hivyo.

68 Sasa, watu wengi, wanafikiri ya kwamba mtu anayeona maono anapaswa kuwa wa Kiungu. Hapana, bwana, sivyo hata. La, bwana. Hakuna wa Kiungu ila Mungu. Ni hayo tu. Wala hakuna mtu . . . Hakuna tofauti kati yetu. Sisi sote ni wenye dhambi, tumeokolewa kwa neema. Wala mmoja hamzidi mwingine. Mtu anapewa tu kitu, naye atalazimika kuwajibika kwa kile alichokifanya na talanta ile aliyopewa. Hiyo ni kweli. Kila mtu anapaswa kuwajibika kwa hilo.

69 Sasa, ninaweza kuwaambia ono ambalo limetukia hivi majuzi. Na kwa hiyo hilo . . . Ndugu Joseph aliniomba nifanye hivi, ili watu walioko humu jengoni ambao hawakuweza kupata to—toleo la gazeti hili, wangeelewa. Nilifanya . . . Nilipokuwa m—mtumishi wa Bwana kwa mara ya kwanza, kuwaombea watoto Wake wagonjwa, mnaijua hiyo hadithi, jinsi alivyoniambia kwamba nilizaliwa nipate kuwaombea wagonjwa.

70 Sasa unasema, "Loo, nimesikia hayo mara nyingi, ambapo, ya watu mbalimbali." Hiyo ni sawa. Mnaona? Kwamba,

wao, si—siwezi kumjibia mtu mwingine. Inanibidi kuwajibika mwenyewe, nawe uwajibike kwa nafsi yako. Sasa hiyo ni kweli.

71 Ndipo aliponiambia hivyo, nilijua ya kwamba kulikuwa, katika huduma hii, ingebidi kuwe na mambo mengi yanayozingatiwa; pesa, kwanza kabisa. Vema, nilimwahidi Mungu, ya kwamba nisingechukua pesa za watu. Nami nikamwomba . . . Sikutaka pesa za watu, lakini nilijua, katika hilo, kungekuwa na pesa nyingi sana nitakazopewa, na itanibidi kuzikataa. Kwa hiyo, nikamwambia, maadamu Yeye alifanikisha njia zangu, isije ikanilazimu kuomba pesa, ningebaki hudumani maadamu Yeye alinifanikisha. Lakini alipofikia ambapo hakunisaidia, ambapo ingetubidi kuomba, ama kuchukua saa nyingi, ama chochote wanachofanya kuchukua sadaka, kama nilivyokuwa nimeona mara nyingi katika kanisa langu la kimadhehebu nililokuwa mfuasi wake wakati huo, basi nikasema ni—ningeondoka hudumani. Alinibariki kwa takriban miaka tisa. Lakini huko California ilininii . . .

72 Huduma yangu, ilionekana kana kwamba, ilianza kushuka, kwa namna fulani. Barua zikapungua. Ilionekana kana kwamba watu hawakujali. "Vema," nikawazia, "Mungu, hayo yote yako mkononi Mwako." Ambapo, nilikuwa nikipata takriban barua elfu moja kwa siku, ama kitu kama hicho, na ziwe chini kule, zingeshuka hadi mia sita, kisha mia tano, kisha zishuke hadi mia nne, mia tatu, mia moja, hadi sabini na tano, mahali fulani. Zikashuka kufikia kama kiwango hicho, kwa siku, barua sabini na tano kwa siku, labda.

73 Vema, nikawazia, "Vema, sijui imekuwaje? Sijui kama nimefanya chochote. Ikinibidi kuninii—kuninii, kwa watu, mbona, sa—sa—samahani." Bila shaka, nikawazia, "Naam, sina . . . Siuzi vitu. Na kitu pekee ambacho watu huniandikia ni kuwapelekea vitambaa vya maombi. Wala hatuviuzi. Tunawapa. Kwa hiyo, vema, Bwana, labda unajitayarisha kubadili mambo."

74 Nikaenda California, nikafikia deni la kama—kama dola elfu kumi na tano, kwenye mkutano. Basi usiku huo, nilipoondoka, nilimwomba Billy aniambie. Nao watu wapendwa waliokuwa wanaifadhili, wakachukua jukumu la kuilipia, nalo lilikuwa ni jambo zuri, zuri sana. Lakini hiyo haikuwa ndiyo ahadi. Nilimwahidi Mungu nitakayofanya.

75 Ndipo wakati ndugu mpendwa aliponipeleka nyumbani usiku huo, huko nje kwenye kibanda kidogo nilimokuwa nikikaa, nilipanda mlimani, niwe peke yangu, yapata saa nane usiku. Nasi tulipaswa kuondoka kwenye saa kumi na nusu. Nami nikaomba, huku mwezi unamulika chini, mwangavu. Naweza kuuona tu. Ilikuwa ni majira ya kupukutika yaliyopita. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, sasa mimi na—naondoka hudumani. Naenda nyumbani. Na lolote unalotaka nifanye tangu sasa, Wewe nifunulie tu."

76 Na kwa hiyo nisingemwambia Billy na hao wengine. Sikutaka kuwaambia, sikutaka kumwambia mke wangu. Lakini, "Loo," nikasema, "Nitawaambia nitakapofika Arizona." Vema, kisha nikasema, "Nitasubiri hadi nifike jimbo zuri la kale la Texas, anakotoka mama yangu." Nikasema, "Nitawaambia huko." Ndipo basi nikafika huko. Nikawaambia nilipokuwa nikiingia Jeffersonville, Indiana.

Vema, Billy, akasema, "Baba, afadhali uwe mwangalifu kwa yale unayofanya." Kasema, "Hivi Biblia haisemi, 'Ole wangu nisipoihubiri Injili'?"

77 Nikasema, "Kamwe sikusema lolote kuhusu kuhubiri Injili. Ninamaanisha huduma ya uinjilisti." Nami nikasema, "Angalia, Billy," nikasema, "Mungu anao watu hudumani, kila mahali. Hanihitaji huko nje. Ninaweza kurudi na kuichukua kazi yangu tena, na—na kuanza uchungaji, na kuichunga maskani, ama kitu fulani. Ninaweza kushuka, nikodi ule ukumbi wa michezo ya kuigiza wa kale huko, nifanye mkutano wa kimataifa wa Jumapili alasiri, na matangazo au kitu kingine." Nikasema, "Siwezi kuacha, mara moja sasa, kwa sababu gharama zangu zinafikia takriban dola mia moja kwa siku, nyumbani. Kwa hiyo, si—siwezi, na ofisi yangu na kadhalika." Nikasema, "Siwezi tu kufunga mara moja, kwa sababu siwezi kulifanya."

Na kwa hiyo mke wangu akasema, "Billy, natumaini unajua unachozungumzia."

Nikasema, "Naam, sasa, na—najua jambo moja."

78 Ninapokuja hapa wakati mmoja katika mkutano mkuu, kwa mkutano mkuu, nanyi mnajua hadithi hiyo, kwa sababu nilimwahidi maskini huyu rafiki yangu Mswidi hapa, Ndugu Boze, kwamba ningekuja na kumhubiria siku mbili, katika Kanisa la Filadelfia, baada ya mkutano huo kwisha. Nami niliambiwa, ikiwa sikufanya; kama kweli ningefanya hivyo, nisingeweza kuwa mnenaji. Ningeweza kujichagulia. Nikasema, "Nitabaki pamoja na neno langu." Nami nikamwendea Ndugu Joseph. Hasa. Kwa sababu, ningefanya hivyo tena. Mtu ambaye hatatimiza neno lake si mzuri sana.

79 Hivyo ndivyo ninavyomchukulia Mungu. Yeye alitoa Neno, nami ninaamini kila Neno Lake. Na kama asingeweza kulitimiza, isingekuwa ni Mungu, kwangu mimi. Mimi . . . Hana budi kulitimiza Neno Lake, naamini. Naye atafanya hivyo, nami najua atafanya. Sasa, ndipo mimi . . .

80 Usiku huo, nilienda kitandani tulipofika nyumbani. Mke wangu alikuwa akilia. Akasema, "Billy, nahofia unafanya makosa." Kasema, "Unajua nataka uwe nyumbani pamoja nami na watoto. Lakini," kasema, "Bill, angalia yale limefanya. Imesababisha uamsho wa ulimwengu mzima, wala siwezi kuona ambapo Mungu angekuleta humu, akutoe hudumani."

Nami nikasema, "Vema, nilimwahidi. Akasema . . . "

"Lakini—lakini—lakini hakukwambia kamwe."

81 Nikasema, "Lakini, nilimwahidi. Unaona? Jambo ndilo hilo. Nilimwahidi. Nitamtimizia neno langu. Kama nitalitimiza kwa ndugu zangu, hakika ningelitimiza kwa Mwokozi wangu." Kwa hiyo niliingia na kulala vizuri sana usiku kucha.

82 Kesho yake asubuhi, yapata saa kumi na mbili, tukaamka. Na—nami nilikuwa tu nikitoka kitandani. Alikuwa upande wa pili. Nilikuwa tu nikiusugua uso wangu, *hivi*. Nikasema, "Vema, nitaipigia simu Kampuni ya Utumishi wa Umma leo, na kuuliza kama ninaweza kurejeshewa kazi yangu ya zamani tena." Nami nikasema, "Wasiponipa kazi yangu, Bw. Wood ni mkandarasi, nitaenda tu pamoja naye. Nami pamoja naye tutatoka tukabomoe baadhi ya majengo, ama kitu fulani. Nami sina budi kufanya kazi, kwa sababu inanibidi kwenda kufanya kazi. Na kwa hiyo, maana pesa hizi hazina budi kupatikana, nami nina deni la dola elfu kumi na tano." Nikasema, "Basi nifanye nini? Sina budi kulilipa hilo, haidhuru walichukua jukumu la kulilipa jinsi gani, ni—nitalilipa. Hiyo ni kweli."

Na kwa hiyo mke akasema, "Utampigia simu Bw.—Bw. Bar, asubuhi ya leo?"

83 Nikasema, "Naam. Nitampigia simu na kumwuliza kama ninaweza kurejeshewa kazi yangu. Na kama yeye. . .Ikiwa kazi hiyo, mtu mwingine anayo sasa, wala hawawezi kumpa kazi bora zaidi," nikasema, "basi nitaninii tu. . .Nitaambatana na Ndugu Wood, nasi tutaanza kujenga mijengo au chochote kile. Nitamsaidia." Na kwa hiyo nikasema, "Nikitoka hudumani, bila shaka, hiyo itamwondosha, pia, naye anaweza kurudi kwenye ukandarasi, nasi tunaweza kwenda kufanya kazi." Hivyo basi wakati. . .

Akasema, "Vema, ha—hakika natumaini unajua unachozungumzia, Bill."

Nami nikasema, "Naam, mimi. . . "

Nami nikatazama. Ikija, ikishuka chini kutoka darini. . . Loo, labda huenda ikawa. . .

Nisingewatarajia mwelewe hilo. Lakini hilo ni jambo ambalo, tutakapokutana katika. . .uso kwa uso na Yesu, mtaninii. . .?. . .juu ya Neno.

Hiki hapa kitu fulani kinakuja, kikijongea. Niliwaona watoto wawili wadogo, wenye nyuso nyeusi wakija, wakishuka chini, wakivuta mkokoteni mdogo.

Nikasema, "Mpenzi, angalia, wakija *hapa*." Nilikuwa nimekwisha kuondoka wakati huo.

Naye akasema, "Unazungumzia nini?" Ningeweza kumsikia, lakini nisingeweza kumjibu.

Na watoto hawa wadogo walikuwa wakinijia, wadogo, kidogo wana nywele ndefu; na macho meusi, kabisa; uso wa kahawia, wakitembea, wakinijia.

84 Ndipo ni—nikawaona basi, nikaanza kwenda mbele. Nikawapita hao watoto, nikamwona Bw. Arganbright, ndugu yangu, ambaye amekwenda ng'ambo pamoja nami mara nyingi, nikamwona amesimama pale, akinitazama. Nikamwendea, yeye.

Sasa, bado niliweza kumsikia mke wangu akitembea-tembea chumbani.

85 Nitalisema hivi ili mpate kuelewa. Huenda yasiwe maneno sahihi, lakini ili mpate kuelewa. Kiwango hicho nilichokuwamo, nilikuwa nimehama basi nikaingia kingine. Nisingeweza kumsikia akitembe-tembea tena. Ilikuwa imekwisha.

86 Ndipo nikamwona Bw. Arganbright. Alikuwa maskini njia yake ya kipekee, jinsi anavyoshikilia kichwa chake na kidogo anatabasamu anaponitazama. Naye akasema, "Ndugu Branham," akasema, "tumesambaza kadi, kila mahali. Na tuna njia kwa ajili yako, kuingia na kutoka. Na kila kitu kiko tayari."

Nikasema, "Vema, Ndugu Arganbright, nitapitia njia gani?"

Akasema, "Endelea mbele tu."

Nikazidi kutembea. Nikawapita baadhi ya wahudumu.

Kisha, nikaenda mbele kidogo. Nikaingia kwenye mandhari kubwa, na kila namna, ilivyoonekakana, wameketi maelfu ya watu.

Na mara nikasikia mtu akisema, "Mkutano umefungwa."

87 "Vema," nikasema, "ni nani aliyeufunga? Ilikuwaje ukafungwa?" Nami nilikuwa nikihoji. Nikasema, "Kwa nini umefungwa? Imekuwaje?" Na kulikuwa na manyunyu.

Ndipo kitu Fulani kikaniambia, "Kwa hili utajua."

Halafu basi nikasema, "Vema, sininii . . . "

88 Ndipo nikaingia, zaidi kwenye hilo ono. Basi lilipofanya hivyo, nilikuwa nimesimama na, mwajua, kiatu kidogo cha mtoto mchanga, wa umri wa yapata mwaka mmoja. Mnajua, maskini vile vijitundu; sio buti dogo, lakini ki—kiatu. Nami nilikuwa na ka—kamba mkononi mwangu, nikijaribu kuingiza tundu hili la moja kwa nane ya inchi kwenye kijitundu hiki, kwa kamba ya karibu nusu-inchi. Nikijitahidi sana, nikijaribu kusukuma kamba hiyo iingie, kamba hiyo ya nusu inchi, kupitia tundu la moja kwa nane ya inchi. Nami nilikuwa nazivunja hizo nyuzi kotekote, hiyo kamba, nikijaribu kuisukuma ipite namna hiyo. Wala isingeingia. Nayo hiyo kamba ilikuwa ikichanika sana, nchani.

89 Kwa hivyo, mara nikamsikia Mtu akisema, nyuma yangu, "Je, huelewi kwamba huwezi kuwafundisha watoto wachanga

mambo ya kimbinguni?” Nikaangalia pande zote. Nayo ilikuwa nyuma yangu. Nami nikaitambua Sauti hiyo. Akasema, “Unatumia ncha isiyofaa ya hiyo kamba.”

90 Ndipo nikaangalia chini mwishoni mwa hiyo kamba iliyokuwa sakafuni, lundo kubwa la kamba, nayo ilikuwa imefungwa vizuri kufikia moja juu ya nane ya inchi, ipate kupitia kwenye lile tundu. Nikasema, “Naelewa.”

91 Basi niliponyosha mkono kuichukua hiyo kamba, nilichukuliwa tena. Sasa, zingatieni hili. Liangalieni likija kutimia. Mnaona? Basi ni—nilipoanza kunyoosha mkono, nilihamishwa tena. Ndipo, nilipojirudia, nilikuwa nimesimama kando ya ziwa la kupendeza, kitu kama vile ziwa lenu hapa nje wakati wa kiangazi wakati ni zuri na la kijani kibichi. Basi kulikuwa na wavuvi pande zote za hilo ziwa, nao walikuwa wakivua samaki, lakini walikuwa wakivua samaki wadogo. Ndipo nikaangalia ziwani, na hao samaki wakubwa, wazuri wa upinde wa mvua huko nje, nami nikasema, “Najua hili ni ono, lakini siwezi kuelewa wale samaki wa upinde wa mvua. Lakini,” nikasema, “mwajua, ninaamini, kwenye kilindi cha moyo wangu kabisa, ninaweza kuwashika hao.” Kwa hiyo, nikachukua hiyo kamba, lakini, badala ya kuwa kamba, ilikuwa ni ufito wa kuvulia.

92 Ndipo papo hapo Yule aliyekuwa nyuma yangu akasema, “Sasa nitakufundisha kuvua samaki, jinsi ya kuwashika hao.” Ndipo basi Yeye akachukua . . . Naye akasema, “Funga chambo.” Basi nikafunga chambo upesi. Akasema, “Sasa itupe huko mbali,” sasa sikilizeni kwa makini, “huko mbali sana kilindini.” Naye akasema, “Ukifanya hivyo, sasa acha chambo kizame ndani, kwanza. Kisha,” kasema, “ivute polepole.” Sasa, hizo kweli ndizo mbinu za wavuvi. Kwa hiyo mimi . . .

93 Akasema, “Halafu, ukifanya hivyo, sasa, utasikia unyofozi kidogo kwake, lakini usimwambie mtu yeyote kile unachofanya. Liweke moyoni.” Kisha kasema, “Ndipo u—ukisikia ikinyofolewa tena,” kasema, “ivute tu kidogo, kidogo, lakini si kwa nguvu sana,” Akasema, “ndipo basi itakivuta mbali na hao samaki wadogo. Nao watakapotawanyika, hilo litavutia usikivu wa hao samaki wakubwa, nao watakinyakua.” Kisha akasema, “Ndivyo utakavyomkamata.” Kasema, “Halafu, wanapouma, mara ya tatu, weka ndoano yako ipate ku—kukamata.”

Nami nikasema, “Naelewa.”

Kasema, “Lakini kimya. Usimwambie mtu yeyote. Kimya.”

Nami nikasema, “Vema.”

94 Nami nilikuwa na hicho chambo mkononi mwangu. Ndipo wavuvi hawa wote wakatokea kuwa ni wahudumu, basi wote wakakaribia, wakisema, “Ndugu Branham, najua unaweza kuwakamata samaki.”

95 Loo, bila shaka, hilo lilinifanya nijisikie vizuri sana. Nikasema, "Loo, naam, mimi ni mvuvi. Ninaweza kuwakamata samaki." Naye akasema . . . Nikasema, "Sasa, hivi ndivyo unavyofanya." Nami nikasema, "Unairusha huko mbali kabisa." Nami nikatoka nje, hadi kwenye—kwenye maji ya kilindi. Nikasema, "Sasa, hao samaki wadogo ni sawa, ndugu, lakini tunataka wale wakubwa, pia." Nami nilikuwa . . . basi . . . Nikasema, "Vema, mnaona, inapozama ndani, sasa angalieni, hiyo hapo, karibu tu na mahali inapopaswa kuwa, sasa, mnaona huko kuna, mnaona, huko—huko, hao ni samaki wadogo." Nikasema, "Sasa, inapotulia tena . . . "

96 Nikaivuta kwa nguvu sana, na, nilipofanya hivyo, nilitoa chambo chote majini. Basi nilipofanya hivyo, nikakamata samaki mmoja, lakini nikashangaa jinsi alivyopata kukimeza chambo kinywani mwake. Maana, ilionekana kana kwamba ngozi ilivutwa juu ya hicho chambo, karibu ukubwa ule ule wa chambo. Nami nikawazia, "Loo, jamani!"

97 Na papo hapo, Huyu aliyekuwa akizungumza, nyuma yangu, akaja mbele yangu. Ilikuwa ni Yeye, Malaika wa Bwana. Alikuwa amekunja mikono Yake. Akanitazama, akasema, "Kile kile nilichokwambia usifanye!"

Nami nikasema, "Naam. Hiyo ni kweli."

98 Akasema, "Unaona, Mvuto huo wa Kwanza ulikuwa ni wakati ulipokuwa unaweka mikono yako juu ya watu na kuwaambia shida yao." Kasema, "Mvuto wa Pili ulikuwa wakati ungejua siri za moyo, kama nilivyokwambia." Kisha kasema, "Badala ya kuweka hilo moyoni mwako, ulijaribu kueleza yote juu yake, na kuwaambia watu. Na ulipofanya hivyo," kasema, "hukujua lolote juu yake, wewe mwenyewe. Basi ungewezaje kulielezea? Nawe umesababisha kuzuka kwa kundi kubwa la uigaji wa kimwili, nawe unaona yale umefanya."

Nami nikasema, "Bwana, kunradhi." Nami ni—nikasema, "Loo, ninasikitika sana! Sijui la kufanya."

99 Nami nilikuwa nikivuta ugwe wa kuvulia, namna *hii*, nami nilikuwa nikijaribu kunyoosha ugwe wangu. Naye akaniangalia, akasema, "Sasa, usiuzongezonge ugwe wako, katika nyakati za namna hii."

100 Nikawazia, "Labda atanipa nafasi nyingine nijaribu tena." Nami nilikuwa . . . Nikasema, "Hakika nitakuwa mwangalifu." Nami nilikuwa nikiupinda ugwe wangu ndani, nikaona umekuwa sawa.

101 Halafu basi wakati aliposema hivyo, mara nikajisikia nikipanda juu zaidi, juu kabisa. Ndipo nilipoketi chini, basi nilikuwa chini, nalo hema kubwa mno, lilikuwa juu. Sijawahi kuona hema kama hilo!

102 Nami nilikuwa ndio kwanza nitoe wito wa madhabahuni, ilivyoonekana, pale chini madhabahuni. Ndipo nilipokuwa kule chini, nilitazama, na kulikuwako na mamia ya watu wamesimama madhabahuni, wakilia, kwa sababu walikuwa wamemkubali Bwana Yesu. Nao walikuwa tu wakilia, kwa sauti kubwa. Nami nikasema, "Loo, hilo linafanana zaidi nalo, namna hiyo."

103 Ndipo muungwana mkarimu sana akaenda jukwaani, kasema, "Wakati Ndugu Branham akipumzika, kwa dakika chache tu," akasema, "tutafanyiza mstari wa maombi." Kisha kasema, "Kila mtu aliye na kadi za maombi kuanzia namba *fulani*, simama huku, upande wa kulia." Vema, nikaona huo mstari wa maombi, ilionekana kana kwamba ulilizunguka hema lote, na kutoka nje, na chini barabarani. Mstari mkubwa mno wa maombi!

104 Nami nikatazama, ambao ulikuwa basi mkono wangu wa kushoto; na hiyo ingekuwa ni mkono wangu wa kulia, kama ningekuwa nimesimama jukwaani, ungekuwa upande *huo*. Kuna kipande cha turubai kilichonyooshwa hapo. Na nyuma ya turubai hii kulikuwa na jengo dogo la mraba, takriban upana wa futi kumi na mbili na urefu wa futi ishirini, kitu kama hicho. Vema, nilisimama na kuangalia hicho.

105 Nami nikawaona wakimleta mama mmoja, kwenye machela. Na kulikuwako na mama mmoja pale akichukua jina lake na kadhalika, pamoja na . . . kwenye—kwenye karatasi. Na kwa hiyo kuna mtu aliyekuja na kumchukua, na kumsukuma akapita. Ndipo mtu wa pili aliyepita, alikuwa na magongo. Nikawaona wakipitia kwenye jengo hilo dogo.

Na upande wa nje, huyo mama akatokea, akipiga mayowe kwa sauti yake yote, akiisukuma hii machela. Nayo ninii . . .

Kisha kulikuwa na mama mwingine upande wa pili, alionekana kama mwanamke mwenye nywele nyeusi, naye akasema, "Kwani imekuwaje?"

106 Akasema, "Sijui kabisa." Akasema, "Siwezi kukwambia kilichotokea." Akasema, "Nimepooza kwa miaka ishirini. Na, tazama, na—najisikia kama kamwe si—si—sikuwa mgonjwa."

Na papo hapo, akatokea yule mwanamume, akiruka na kuruka-ruka, akiwa na—akiwa ameshika magongo yake mkononi mwake. Basi ni—nikaangalia jambo hilo. Ndipo wakati uo huo . . .

107 Sasa, hili hapa jambo fulani. Angalieni kwa makini. Kuna tofauti kati ya Malaika wa Bwana na Nuru hiyo. Kwa sababu, nilisikia kitu fulani kikijongea, kama ifanyavyo inapokuja hapa jukwaani, usiku, kitu kama "Whiu! Whiu! Whiu!" na kama Moto unaozunguka, ndimi za moto zikiramba. Nayo ikaniacha, kisha ikashuka moja kwa moja juu ya kusanyiko hilo, kisha ikaenda na kusimama juu ya kilele cha jengo hilo dogo, kisha

ikatulia juu yake. Ndipo basi, ilipofanya hivyo, Huyu aliyekuwa amesimama karibu nami, nyuma yangu, Sauti ile ile, Sauti ya Malaika, akasema, "Nitakutana nawe mle ndani. Na huu ndio Mvuto wa Tatu, lakini hakuna mtu atakayejua lolote kuuhusu."

Nami nikasema, "Vema, sielewi. Mbona humo ndani? Mbona humo?"

Akasema, "Halitakuwa onyesho la hadharani, wakati huu."

Nami nikasema, "Sielewi, kuingia kwenye chumba kile cha faragha hivyo."

108 Naye akasema, "Hivi haikuandikwa na Bwana, 'Wewe usalipo, usiwe kama wanafiki wanaopenda kusikilizwa mbele ya watu. Lakini ingia katika chumba cha siri na uombe kwa Baba aonaye kwa siri; Naye aonaye kwa siri atakujazi kwa wazi'?" Ni kulingana na Maandiko kikamilifu. Kila wakati, ndivyo ilivyo.

Nami nikasema, "Naelewa."

109 Kisha akanipeleka mahali hapa, na kuniketisha chini katika chumba hiki nilimokuwa. Ndipo basi akaniambia la kufanya kwa mara ya tatu. Sasa, marafiki Wakristo, hayo, nitakapouacha ulimwengu huu, hayo yatakuwa bado kifuani mwangu. Wakati mimi . . . Lakini, zingatieni maneno yangu, kitakachotokea.

Wakati, hiyo—hiyo ilikuwa miezi mitano iliyopita, miezi sita sasa, nasi hatukujua kabisa tungewahi kwenda huku—huku chini Meksiko.

110 Lakini nilifikiri nilikuwa ninaenda Phoenix. Ndipo rafiki na ndugu yetu mpendwa ambaye anawaombea wagonjwa, Bw. Allen, akaingia mle. Akasema, "La. Nitakaa hapa, kwa hiyo sitaondoka kwenye sehemu hiyo ya mwezi." Vema, nisingeingia mle wakati huo, huku ndugu yangu akiwa mle ndani. Nisingefanya hivyo. Kwa hiyo, simjui Ndugu Allen, lakini hata hivyo anafanya huko nje kazini mwa Bwana. Kwa hiyo mimi . . . Wao wakasema, "La. Alikuwa anaenda kukaa." Nikasema . . .

111 Vema, ndugu waliniita, li—lile shirika huko, kundi la wahudumu. Ambapo, nilipaswa kupachukua mahali pa Ndugu Roberts alipokuwa anaenda Australia. Nikasema, "Vema, hilo ni sawa. Endapo wana mtu kule, Ndugu Allen akiwaombea wagonjwa, nisingeenda. Hilo lisingekuwa la kidugu." Kwa hiyo nikasema, "Vema."

Ndipo Ndugu Arganbright akanipigia simu, siku chache baadaye, na kusema, "Ndugu Branham, nimezungumza na . . . Ndugu Moore. Kwa nini usiende Meksiko?"

Nikasema, "Loo, Baron von Blomberg na wengi wao wamejaribu kunipeleka Meksiko. Sijali kuhusu kushuka kwenda kule."

Nikasema, “Hebu tufanye mkutano wa Kimarekani mahali fulani.” Nikasema, “Nilitaka kupiga hema hilo pale, kwa mara ya kwanza.”

Naye akasema, “Vema, kwa nini tusiende Meksiko?”

Nikasema, “Vema, sawa. Nitaninii . . . Wewe lishughulikie.”

112 Kwa hiyo kulikuwa na mtu mwingine kule chini. Naye akapiga simu tena, akasema, “Mkutano umepangwa kwenye tarehe zizo hizo.” Naye akasema, “Tumeupanga kwenye uwanja mkubwa mno wa michezo huko chini.”

113 Basi usiku huo, nilikuwa chini kwa Bw. Wood. Nikawazia, “Unajua, hiyo ni kweli. ‘Watoto wadogo weusi, wanaofanana na Wahindi,’ ndivyo hilo ono lilivyo.” Ndipo basi nikasema, “Lakini, jambo la kushangaza, ilipaswa kuwa katika mandhari, na kitu fulani kuhusu ‘kuwaruhusu wafumukane.’” Hivyo basi wakati sisi . . .

114 Siku mbili baadaye, Bw. Arganbright akapiga simu na kusema, “Ndugu Branham, tuna uwanja mkubwa wa michezo ya ng’ombe. Nayo serikali ya Meksiko imekuruhusu uingie, kwa mara ya kwanza katika historia ya Meksiko ambapo mtu asiye Mkatoliki aliwahi kuruhusiwa na serikali.”

Kwa hiyo nikasema, “Hiyo ni ajabu sana.” Kwa hiyo nikasema, “Sasa jambo fulani linakaribia kutukia.” Nikasema, “Tuna tatizo linalokuja.”

115 Nanyi mnajua, tuliposhuka kwenda Meksiko na kujitayarisha, na kwenda kwenye huo uwanja wa michezo ya ng’ombe, mtu fulani . . . Ilinyesha, barabarani tukielekea huko nje, na mtu fulani alikuwa ameifunga mikutano hiyo. Wala hawajui ni nani aliyeifunga, bado. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

116 Kisha nikarudi nyumbani, nikarudi kwa ndege kesho yake. Tusingeweza hata . . . Ndugu Moore akasema, “Ndugu Branham, nita—nitachunguza.” Wala tusingeweza hata kupata mhudumu, popote. Wala hakuna mtu aliyejua lolote kulihusu. Ndipo Ndugu Moore akasema, “Kama mimi . . . Ndugu Branham, kadiri nilivyokufuata, kama sijawahi kukuamini kufikia wakati huu, hakika ningekuamini sasa.”

Nami nikasema, “Hiyo ni kweli.” Kwa hiyo, tukarudi huku.

Ndipo basi nikasikia Bw. Arganbright alikuwa njiani kuja kuniona.

117 Nikaenda kuomba kwenye pango langu, na kumwuliza Bwana nini. Akanionyesha ono lingine. Akasema, “Samaki waliokufa.” Walikuwa wamelala, Naye akaniambia ilikuwa ni nini. Kasema, “Rudi. Lakini huu sio wakati hasa, lakini nitaubariki.”

118 Nikarudi kule chini, na mahali fulani karibu watu elfu arobaini, elfu hamsini wakamjia Kristo. Mtoto mchanga aliyekufa akafufuliwa katika wafu, na mambo makuu yakatukia.

119 Sasa ninangojea wakati. Unaweza kuwazia jinsi hili linavyoonekana kuwa dogo sasa, kwamba mambo haya yanatukia, mambo haya makuu ambayo tayari yametukia.

120 Hivi majuzi usiku, mimi, bila kujua. . .Ni wangapi waliokuwa kwenye Kanisa la Filadelfia waliponisikia nikimwambia mtu fulani, "Alaaniwe mtu anayeinua macho yake wakati ninapomwombea mwanamke huyu kipofu"? Hivyo ndivyo nilivyokuwa nikifanya. Mnaona?

121 Bwana anajiandaa kuwatembelea watu Wake, katika jambo kuu la ajabu, marafiki. Nami ningeninii. . .Haina budi kuwa ni siri moyoni mwangu mwenyewe. Lakini kama vile mnavyonijua, na mnaniamini, na kunipenda, na kuniheshimu kama mtumishi wa Mungu; kumbukeni tu, ninawaambia, baraka ziko njiani, hiyo ni kweli, zikija. Wala haitanidhoofisha. Haitawahi kunidhoofisha tena. Na itakuwa kubwa sana kuliko kitu chochote ambacho kimewahi kutokea hapa au wakati mwingine wowote. Ni kitu tu ambacho Bwana ametoa. Nami nataka. . .

122 Hiyo ingenifanya mwenye—mwenye kuamini neema. Baada ya kufanya, na mambo ambayo nilikuwa nimefanya, na jinsi nilivyokuwa nimetenda, na kuhukumiwa mbele za Mungu, na hata hivyo, Mungu anapozungumza chochote na kufanya ninii. . .Atafanya hivyo, kwa vyovyote vile. Amina.

123 Musa alimwua mtu, wakati mmoja. Lakini Mungu alikuwa amedhamiria. Alimhifadhi kule nyuma upande wa nyuma ya jangwa, kwa miaka arobaini, bali aliwapeleka Israeli kwenye nchi ya ahadi.

124 Yeye si ni wa ajabu? Yeye ni Mungu yule yule leo hii ambaye alikuwa wakati huo. Na, enyi marafiki, ninawaambia hili, kila mmoja wenu ninyi waaminio Wakristo, bila kujali unahudhuria kanisa gani.

125 Huko chini kwenye studio, hivi majuzi, kulikuwa na mtu. Nilikuwa nikizungumza naye, mtu mzuri sana pamoja na mkewe, ambapo mimi na Ndugu Boze tulikuwa tukirekodi kwa ajili ya matangazo. Naye alikuwa akinipa mkono na kuzungumza. Nami nikasema. . .Vema, a—anampenda Ndugu Joseph sana. Nikasema, "Wewe. . .Wewe huenda kanisani mwake?"

Akasema, "La. Mimi ni Mmethodisti."

Nikasema, "Vema, unaweza kusamehewa hilo." Na kwa hivyo nilikuwa tu nikimtania, namna hiyo. Ndipo nikasema, "Nilikuwa nikiendelea tu, kwako."

126 Nikasema, "Angalia, ndugu, nilikuwa nikiendesha farasi kidogo. Naye baba yangu alikuwa mpanda farasi." Nami nikasema, "Huko juu kwenye Msitu wa Arapaho, ambako tuliwalisha ng'ombe," nikasema, "wao . . . Hakuna kitu ambacho kingeweza kuja kwenye safu hiyo ila Hereford ukoo safi, kabisa. Msimamizi husimama kwenye huo ua hami wala hataruhusu chochote kupita isipokuwa kiwe ni Hereford ukoo safi aliyesajiliwa." Nami nikasema, "Baadhi yao wanakuja na Goigoi J, wengine wanakuja na Mkuo W, wengine na Mviringo R, wengine na Kiweko. Wamebandikwa chapa tofautitofauti, lakini wote ni Hereford ukoo safi." Hiyo ni kweli.

127 Hivyo ndivyo ilivyo. Tunaweza kuwa Methodisti, Baptisti, *hili*, ama *lile*, ama *linginelo*. Lakini maadamu wewe ni Mkristo ukoo safi, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, hicho ndicho kitu pekee kinachoweza kuingia malishoni, Zizini. Kwa sababu, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Nasi tunakuwa watu wamoja, Kanisa moja, tukiwa na wazo moja na nia moja: kumtukuza Yesu Kristo tukiwa hapa duniani. Mbingu moja! Hiyo ni kweli? Nasi tunashukuru sana kwa ajili ya hilo.

128 Sasa nimepitisha wakati wangu, wa kuongea nanyi, maana inawabidi mharakishe mrudi baada ya muda mfupi. Lakini ni wangapi wanaopenda mazungumzo ya moyo-kwa-moyo? Mnaonekana kuwa mna—mnalielewa. Tungeweza kuzungumza saa baada ya saa.

"Na sasa," kama kusema, "Ndugu Branham, unaweza kunifafanulia hili?" Siwezi. Laiti ningaliweza, lakini siwezi. Haiwezekani.

129 Huwezi kuelezea mambo ya kimbinguni. Nawe unapojaribu kufanya hivyo, ni kama tu vile Yeye alivyoniambia, unasababisha ulinganishi wa kimwili kuibuka. Unaona? Unausababisha. Ni halisi tu. Itafanya hivyo. Na ni—ni kizuizi kwa Mwili wa Kristo. Mnajua ninalomaanisha? Hu—hu—husababisha ugomvi.

130 Sasa, jambo la kufanya ni kuwa mkweli moyoni mwako, umpende Bwana kwa moyo wako wote, na uwe na shukrani tu kwamba Mungu anasonga mbele pamoja nasi, Bwana Yesu Kristo aliyefufuka.

131 Nami nasema hivi, na kufanya ubashiri huu. Silisemi katika Jina la Bwana, sasa. Ninalisema, kama ndugu yenu. Ninabashiri hili. Basi sikilizeni kwa makini. Ninabashiri kwamba Marekani, mwaka huu, Marekani, mwaka huu, ama itampokea Kristo au itaanza kuanguka, kuanzia mwaka huu. Naam. Huu ndio wakati wa Marekani kutubu. Na endapo haitatubu . . . Nilibashiri hilo mnamo, nadhani, yapata Januari 15 au 16 mwaka huu, nikijisikia tu kuongozwa kulisema. Nalo . . . Nimedumu nalo.

132 Nami niliangalia magurudumu yakifingirika. Ninamwona yule mwinjilisti mashuhuri, Billy Graham, alirudi kutoka ng'ambo na akaiandaa mikutano yake, New York na sehemu hizi kuu, kuingia kwenye kiini chenyewe, na kadhalika. Nami naona ya kwamba, Ndugu Roberts alifukuzwa kutoka nchi za kigeni. Bw. Arganbright ananitaka mimi, baada ya Juni, na hao wengine, kwenda Ujerumani, turudie Afrika Kusini na kupitia kule, lakini kitu fulani kinanishikilia Marekani. Na hao wengine wote wanaonekana kuwa vivyo hivyo.

133 Na ninaamini ya kwamba Marekani itapata wito wake wa mwisho, mwaka huu. Kweli. Nisingethubutu. Angalieni *hapa* kwenye kanda *hapa* chini. Zinaweza kuchezwa miaka ishirini kuanzia leo. Mnaona? Inakubidi kuchunga unachozungumzia, uchunge unachosema. Lakini naamini hivyo. Sasa, Bwana hajaniambia jambo hilo. Lakini ninaamini hivyo, ya kwamba ama Marekani itampokea Kristo au itamkataa, kabisa, mwaka huu. Nami nabashiri ya kwamba watamkataa. Ninabashiri.

134 Angalieni wanachofanya huko Florida, kwa Jack Coe. Angalieni wanachofanya, kila mahali. Wangewezaje kamwe . . .? Hiyo hata ni kukiuka katiba, kumfukuza mtu jimboni. Tunayo haki ya kujieleza. Bila shaka, tunayo. Lakini wataninii . . .

135 Muda si muda mwajua, watajaribu kukomesha haya yote. Watajaribu kuacha kuwaombea wagonjwa, na kuweka "marufuku" juu yake. Basi kumbukeni tu ya kwamba: wakati mateso yatakapotokea, Kanisa, litafikia kilele Chake basi. Daima ndiyo bora zaidi. Naam, bwana. Naye Mungu anayatekeleza yote pamoja.

136 [Ndugu mmoja anasema, "Amina. Utukufu kwa Mungu! Amina. Amina. Amina. Amina. Na utukufu kwa Mungu!"—Mh.] Asifiwe Mungu atupaye ushindi!

137 [Dada wawili wananena kwa lugha kwa wakati mmoja—Mh.] Tafuteni tafsiri sasa, tuone yale ambayo angetwambia. [Dada wawili tena wanena kwa lugha kwa wakati mmoja. Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . na kweli.

138 Kuna tafsiri ya kufuata haya sasa. Kila mtu awe na kicho kweli. Na yule mama akanena, yeyote yule. Sikilizeni kwa makini sana. Hebu wale wanaojua, sasa, waone. [Dada mmoja anaanza kunena kwa lugha nyingine—Mh.] Shh, shh, shh, shh, shh! [Dada huyo anaendelea kunena kwa lugha nyingine, huku dada mwingine akitoa tafsiri wakati uo huo.]

139 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mmesikia tafsiri hiyo. Ni wangapi hapa wanaotaka kumpokea Kristo kama Mwokozi binafsi, ili wakumbukwe katika maombi? Je, mnaweza kuinua mikono yenu juu sana sasa hivi? Juu sana, ili tuweze kuona wewe ni nani, juu kabisa.

Tupate sauti ndogo kwenye kinanda, tafadhali, kwa dakika chache.

140 Unapoinamisha kichwa chako sasa, na kuamini kwa moyo wako wote, wakati sauti imesema ya kwamba hii ilikuwa ni Kweli. Ikiwa utawahi kuingia, njoo sasa.

141 Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba, Roho Wako anapotembea juu ya jengo hili sasa. Nazo zile sauti zikatoka na kusema ya kwamba huu ndio wakati, hii ndiyo saa. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba, nikiona mikono hiyo yote iliyoinuliwa. Wengine, labda mikono thelathini ama zaidi, iliinuliwa hewani sasa hivi, kumpokea Kristo kama Mwokozi wao binafsi; wakisikia Ujumbe, wakijua ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

142 Mioto hii ya uamsho kwenye kila kilima. Mungu aliahidi, katika siku za mwisho, ya kwamba angeyainua mambo haya, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, na kati yetu na kufanya yaliyo kweli, na kuonyesha ishara kuu na maajabu miongoni mwa watu, hata vipofu wangeona, viziwi wangesikia, na kungekuwa na huduma kuu za kimbinguni zikiendelea. Na leo, Bwana, tunaishi ili kuiona.

143 Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kila mmoja wa maskini hawa watoto wapendwa, walioinua mikono yao sasa hivi, kwamba walitaka kukupokea Wewe kama Mwokozi wa kibinafsi, kwamba utawaokoa kutoka katika dhambi. Tujalie, Bwana.

144 Nami naomba, pia, ya kwamba tukiwa katika huduma hii kuu sasa hivi, ya kwamba Roho Mtakatifu atajaza kila moyo, upya. Washa moto mpya, Bwana, ndani ya nafsi zao. Jalia watoke nje wenye bidii, baada ya kusikia; mara Neno hilo liliponenwa, kwamba taifa letu tunalolipenda lingeukataa huo mwaliko.

145 Ee Mungu, falme kuu hazina budi kuanguka. Kila kitu kipatikanacho na mauti hakina budi kutoa nafasi kwa ajili ya kutokupatikana na mauti, Ee Mungu, tunapoona hili. Tunasimama kule kwenye magofu ya kale ya Rumi, kuona mahali ambapo ile nchi kuu ya kifalme siku moja ilisimama kama mahali palipochanua pa ulimwengu, sehemu angavu zaidi duniani kote. Na, leo hii, unachimba futi ishirini chini ya ardhi, ili kupata magofu ya ile milki kuu. Huko ng'ambo, pale hekalu liliposimama wakari mmoja, Uislamu wa Omar unasimama. Mengi ya yale mambo makuu, mataifa makuu, Alexander Mkuu, na Ugiriki, na sehemu zingine nyingi, jinsi hizo falme zilivyoanguka!

146 Mungu, tunaona msingi wa taifa letu ukiporomoka, kwa sababu ya kuikataa Injili. Wakati watu mashuhuri wamepitia kwenye taifa hili, wakachambua kila mahali, jumbe za Injili zilisambaa; roho kama Yohana Mbatizaji, isiyofanya miujiza wala kusema lolote juu ya miujiza, bali ilipitia taifa zima. Ndipo nguvu za kutenda miujiza za Yesu zikaifuata, kama ilivyofanya Yohana, na bado taifa letu, wiski, tumbaku, vilabu

vya usiku, dhambi zikilundikana kila upande. Ustaarabu wetu mkuu unaanguka, unaanguka. Kila kitu lazima kitoweke. Falme hizi zote hazina budi kuanguka, ili Ufalme wa Mungu utimizwe, katika mwangaza wake, ndipo ule Utawala wa Miaka Elfu uchukue mahali pake.

147 Kuona mti wa kale, ambapo wakati mmoja, miaka michache iliyopita, kama mvulana, niliketi; wakati matawi yake makubwa, ya kifalme, jinsi nilivyofikiri mti huo ungedumu pale kwa mamia ya miaka. Na leo hii ni kisiki, tukijua kwamba vitu vyote vipatikanavyo na mauti havina budi kuangamia.

148 Mimi pia, Bwana, wakati mmoja nilikuwa kijana mwanamume, najiona nikiondoka sasa, nikifikia juu ya mstari kule, kuona machweo ya jua. Leo hii, vichwa vingi vyenye mvi vimeinamishwa katika jengo hili, ambao wakati mmoja walikuwa vijana wenye nguvu, wenye sura nzuri. Wanawake wengi wakiwa wameinamisha nyuso zao, makunyanzi, na sasa machozi yanakata njia kupitia kwenye hayo makunyanzi usoni mwao ambao wakati mmoja ulikuwa mzuri na wa kupendeza, kama wasichana. Ee Mungu! "Miili yote ni kama nyasi." Mwisho umekaribia.

149 Ee Kristo wa Mungu, wapokee maskini watu hawa katika Ufalme Wako. Siku moja, sina budi kusimama huko Ng'ambo kwenye—kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na kutoa hesabu ya huduma yangu, kutoa hesabu kwa ajili ya mambo haya ambayo umeniruhusu kufanya, Bwana, miongoni mwa watu, kutangaza kufufuka kwa Bwana Yesu. Mungu, sina budi kuwajibikia hilo. Ee Mungu, iwashe bidii moyoni mwangu, zaidi na zaidi, na hekima, nipate kujua jinsi ya kuwaongoza watu kwa Bwana Yesu.

150 Leo, Baba, umeahidi katika Neno Lako Takatifu, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

151 Mikono mingi hapa iliinuliwa, Bwana. Maskini watu wengi waliopotea, wengi wao walirudi nyuma na kuondoka njiani. Mungu, jalia kwamba, dakika hii tu, kwamba Roho Mtakatifu akishuhudia kwamba mambo haya ni kweli, ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho, nao wanatambua ya kwamba siku moja hawana budi kuondoka. Jalia wampokee Kristo sasa hivi, huku tumeinamisha vichwa vyetu.

152 Je, kuna mtu hapa ndani sasa, ambaye hakuinua mkono wake kwenye wito wa kwanza? Je, ungeweza kuinua mkono wako sasa? Na kusema, "Ninataka kumpokea Kristo, wakati huu, kama Mwokozi wangu." Je, waweza kufanya hivyo? Mtu mwingine? Ambaye kamwe . . .

153 Je, mliona jinsi Moto ulivyolipiga hili jengo wakati Neno hilo lilipotokea? Mnaona? Ninaamini, rafiki. Mungu akubariki,

rafiki yangu kijana, kijana mwanamume uliyeinua mkono wako. Mungu, mjalie ndugu yangu. Unao Uzima wa Milele kwa kumwamini Bwana Yesu.

Nashangaa, katika roshani mahali fulani?

154 Kama tunaona kwamba Mungu aliahidi mambo haya, tuko hapa kuyaona yakitimia. Tunajua kwamba Mungu aliahidi hayo. Na chochote anachoahidi Mungu, Mungu anawajibika kukifanya.

155 Kunaweza kuwa na mwingine? Mungu akubariki, mama. Ninauona mkono wako. Mtu mwingine anaweza kuinua mkono wake? Mungu akubariki, mama. Nauona mkono wako. Mungu akubariki, msichana. Naona mkono wako. Mtu mwingine? Mungu akubariki, mama. Naona mkono wako.

156 Mtu fulani kwenye roshani? Ningependa kuona mtu fulani, juu kwenye roshani, ambaye si Mkristo, angependa kusema. Mungu akubariki. Nilijua tu ulikuwa huko juu, mwanangu. Kuna mtu fulani, kwa sababu Roho Mtakatifu alionekana kuniongoza kwenye roshani. Sijui ni kwa nini. Mimi si mlokole. Ikiwa ndivyo nilivyo, simaanishi kuwa. Lakini inaonekana tu kama kulikuwa na mtu kwenye roshani. Mungu akubariki, mwanangu. Naomba wewe. . .Na kama huyo ni mke wako karibu nawe, naomba ukamtumikie Bwana Yesu kwa moyo wako wote. Na abadilishe maisha yako, nyumba yako. Ataibadilisha. Na uwe mtumishi Wake.

157 Kuna mtu mwingine, kabla tu ya kufunga sasa, kabla sijamkabidhi Ndugu Boze ibada? Wavulana hao itawabidi waingie, kwa dakika chache, na kuanza kusambaza kadi za maombi. Je, mnaweza, mmoja tu zaidi, kuinua mkono wao, mahali fulani jengoni? Ndugu Joseph. . .Laiti ungeinua mkono wako, kwa muda kidogo tu; ninataka kuomba pamoja nanyi, tena. Naam. Mungu akubariki. Nakuona hapo chini. Asante, bwana mwema. Mungu akubariki hapo, ewe kijana. Hilo ni zuri sana.

158 Sasa, hili linaweza kuonekana geni kidogo kwa baadhi yenu, jinsi ambavyo Neno hilo moja lingevunja kitu kama hicho, nao Moto utawanyike. Mnaona? Ni kwa sababu ni Kweli, ja—jambo kuu kwa Ujumbe, mnaona, kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

Mungu akubariki, bwana. Nauona mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

Sasa, ninawaambia, enyi marafiki, kuna wengi wanaoketi hapa, ninaamini, ambao watastahimili mateso ya kutisha kwa ajili ya imani yao kabla haijatiwa muhuri.

159 Mungu akubariki. Mtu mwingine anainua mkono wake? Mungu akubariki, huko nyuma kabisa. Ninauona mkono wako, bwana. Mtu mwingine? Sasa, mtu mwingine, inua mkono

wako upesi sana. Tunapongojea maombi ya kufumukana, kama utainua mkono wako. Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Ninauona mkono wako, juu ya mtu huyo kule juu. Naam. Mungu akubariki, ndugu. Naona.

160 Hilo ni zuri sana; ndio kwanza umkubali Kristo. Wewe, unapoinua mkono wako, Mungu analiandika kwenye Kitabu cha Uzima. Dakika ile ile unapoamini, unapita kutoka mautini kuingia Uzimani, unapoinua mkono wako. Uliinuaje mkono wako? "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, kwanza." Ndivyo hivyo. Mungu, hapa, akivuta; unainua mkono wako. Malaika wakiandika jina lako kwenye Kitabu cha Uzima. Hilo latosha. Sasa utampokea Roho Mtakatifu ikiwa tu utaamini.

Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa tena.

161 Baba yetu wa Mbinguni, tuma baraka Zako. Nami nakushukuru, Baba, kwa ajili ya kundi hili kubwa la watu ambao ndio kwanza wampokee Kristo. Ninakushukuru kwa kuuthibitisha Ujumbe Wako, Bwana, na kuutoa, na kufanya mambo ambayo umetufanyia leo. Watu hawa watakuwa na furaha siku zote za maisha yao. Umewapa Uzima wa milele, sasa hivi, kwa sababu wamemwamini Bwana Yesu. Tena, Baba, wito huo wa madhabahuni unapofanywa, kwa muda mfupi tu, kuja hapa na kusimama kibinafsi madhabahuni au kwenye marefu ya kanisa, na kukuomba Wewe na kushukuru kwa wokovu wao, ninaomba ya kwamba kila mkono ulioinuliwa utasimama kwenye marefu ya kanisa, mahali fulani, na kukuomba Wewe, na kushukuru kwa kuwapokea ndani, au, kuwapokea katika Ufalme Wako. Tujalie, Bwana. Baraka Zako za Milele na zikae juu yao.

Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, Ndugu Joseph ataendelea, maombi.

56-0408A Ono Ni Nini?
Lane Tech High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org